


Jeje, ni nini unachotarajia?

# OMBI LANGU LA HIFADHI

Huku ukisubiri uamuzi, **usiende** katika nchi nyingine bila idhini.

- Ikiwa huwezi kurudi katika nchi yako kwa sababu si salama kwako, **unaweza kuomba hifadhi hapa**.
- Hifadhi pia inajulikana kama **ulinzi wa kimataifa**.
- **Mtoto (chini ya umri wa miaka 18)** aliyewasili peke yake anapewa mtu anayejulikana kama **mlezi** kwa ajili ya kutoa msaada.
- Baada ya kukkagua taarifa zote, mamlaka zitaamua **ikiwa unahitaji hifadhi au la**.

## USAJILI

- Mamlaka zitasajili ombi lako, kupiga picha yako na kuchukua alama za vidole (ikiwa una umri unaozidi miaka 6) na kukagua hati zako.
- Utapewa hati inayoonyesha kuwa umeomba hifadhi. Ihifadhi salama.
- Baada ya usajili, utapokea mwaliko wenye tarehe, saa na eneo la mahojiano.

## UKISUBIRI MAHOJIANO YAKO

- Utaishi mahali salama. Huku ukisubiri, jaribu kujishughulisha.
- Jifunze lugha ya wenyeji, pata marafiki wapya, cheza michezo na hakikisha kuwa una afya nzuri.
- Omba mshauri wa kisheria au mlezi wako akusaidie kujiandaa kwa ajili ya mahojiano hayo.



Usikose mahojiano yako ya kuomba hifadhi! Ikiwa wewe ni mgonjwa, ijulishe mamlaka.

## MAHOJIANO YAKO YA KUOMBA

- **Utaulizwa kwa nini uliondoka nchini mwako**, kuhusu familia yako, maisha yako ya nyumbani na safari yako.
- **Beba hati** (kitambulisho, picha, stakabadhi) ili kuthibitisha hadithi yako.

## UAMUZI

**Baada ya miezi michache**, utapokea uamuzi.

- **Ikiwa unmepewa hifadhi**, unaweza kuishi katika nchi hii na kuhamia katika makazi ya kudumu zaidi.
- **Ikiwa imekataliwa**, utaarifiwa kuhusu chaguo salama za kurejea nyumbani. Ikiwa hukubaliani na uamuzi huo, unaweza kuupinga kirasmi. Hii inaitwa kukata **rufaa**.

## KUMBUKA

- Unaweza kumuona wakili ili kupata ushauri kuhusu kurejea nchini mwako au jinsi ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi hunaokukataza hifadhi.
- Omba mkalimani ikiwa huzungumzi lugha hiyo.
- Ikiwa huwezi kujibu maswali ambayo afisa huyo anakuuliza, unaweza kusema hivyo.
- Maafisa wote lazima wakutendee kwa heshima.
- Shirikiana na maafisa hao. Waombe waeleze wanachomaanisha ikiwa jambo lolote wanalosema halieleweki.



© Shirika la Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Hifadhi, 2025

euaa
EUROPEAN UNION AGENCY FOR ASYLUM